WASIFU WA HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA (DISTRICT PROFILE) KWA MWAKA 2016.

1. UTANGULIZI

1.1 Jiografia

Wilaya ya Rorya ilianza rasmi tarehe 01/07/2007 baada ya kugawanywa kutoka Wilaya ya Tarime. Wilaya ipo kaskazini mwa Tanzania kati ya latitude 1^{o} .00″ - 1^{o} 4.5″ Kusini mwa mstari wa Ikweta na Longitude 33^{o}· 30″ - 35^{o}·00″ Mashariki mwa mstari wa Meridiani. Wilaya ina ukubwa wa kilomita za mraba 9,345.496 ikiwa eneo la maji (Ziwa Victoria) ni kilomita za mraba 7,252 sawa na asilimia 77.6 ya eneo la wilaya. Eneo la nchi kavu ni kilomita za mraba 2,093.496 sawa na asilimia 22.4 eneo wilaya. Wilaya inapakana na nchi ya Kenya Kwa upande wa kaskazini, Wilaya ya Tarime upande wa Mashariki. Wilaya za Butiama na Musoma kwa upande wa kusini na Nchi ya Uganda upande wa Magharibi.

1.2 Muundo wa Utawala

Wilaya ya Rorya ina jumla ya Tarafa 4, Kata 26, Vijiji 87 na Vitongoji 506 na kaya ikiwa Kata 24 katika Halmashauri ya Wilaya na Vijiji 87 na Mamlaka ya Mji Mdogo Shirati in Kata 2 na vitongoji 9.

1.3 Idadi ya watu

Kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka **2012,** Halmashauri ya Wilaya ilikuwa na wakazi 265,241 ambapo kati ya hao wanaume wlikuwa 126,247 (47%) na wanawake walikuwa 138,994 (53%); na kwa wa wastani wa ongezeko la watu (Population growth Rate) la asilimia 2.8, Wilaya ya Rorya inakadiriwa kuwa na wakazi 295,197 kwa mwaka 2016. Kati ya hao wanaume 140,505 na wanawake ni 154,692. Kutokana na idadi hii ya wakazi, inakadiriwa msongamano wa watu kwa kilometa moja ya mraba kuwa ni 125.

1.4 Uchumi wa Wilaya:

Uchumi wa Wilaya ya Rorya unategema hasa shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi. Aidha Mazao makuu yanayolimwa Wilayani ni Mahindi, Mihogo, Migomba, Mtama, Ulezi, Viazi vitamu, Maharage na mazao ya Biashara ni kahawa, Pamba na alizeti. Shughuli kuu za kiuchumi za wakazi wa Wilaya ya Rorya ni ;

- Sekta ya Kilimo na ufugaji inaajiri takribani asilimia 91 ya wakazi wote.
- Sekta ya Uvuvi huajiri asilimia 3.44 ya wakazi wote.
- Biashara ndogondogo huajiri asilimia 5.42 ya wakazi.
- Shughuli nyinginezo takribani asilimia 1.14 ya wakazi.

1.5 Hali ya Hewa

Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ipo katika mwinuko wa mita 800 hadi 1,200 juu ya usawa wa Bahari. Mtazamo wa ardhi ya Halmashauri ni rasi, ghuba, miteremko, tambarare, mawe yaliyojitokeza na mito inayomwaga/peleka maji katika ziwa

Victoria. Kiasi cha mvua na hali ya hewa inatofautiana kutokana na umbile la ardhi eneo kwa eneo na mvuto wa ziwa. Kiasi cha mvua kwa mwaka ni kati ya mm 700 hadi 1200 kwa mvua inayonyesha misimu miwili.

Mvua za msimu wa vuli huanza mwezi Oktoba hadi Desemba na mvua za masika huanza mwezi Machi hadi Juni. Hali ya hewa ni ya joto la kadri, lenye vipimo vya nyuzi joto kati ya nyuzi 14^0C hadi 30^0C. Aidha Wilaya imegawanyika katika kanda mbili za kilimo kama ifuatavyo: -

Jedwali Na 2 ni kanda kuu za kilimo

UKANDA	MWINUKO	KIASI CHA MVUA	MAZAO MAKUU	
			Mazao ya chakula	Mazao ya Biashara
KATI	Mita 1,000 – 1,200	Mm 700 – 1,200	Mahindi, Mihogo, Migomba, Mtama, Ulezi, Viazi vitamu, Maharage	Kahawa, Alizeti
CHINI	Mita 800 – 1,000	Mm 700 – 900	Mahindi, Mihogo, Migomba, Mtama, ulezi, Viazi vitamu, Maharage	Pamba, Alizeti

Chanzo Afisa kilimo, Umwagiliaji na Ushirika

2. HALI YA WATUMISHI

2.1 Rasilimali Watu

Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ina jumla ya watumishi 2,615 wa kada mbalimbali. Idadi hii inajumuisha watumishi wa Makao makuu, ugani, Waganga na watendaji wa Vijiji na Kata, na walimu walioko vijijini. Aidha idadi hii ni ndogo ukilinganisha na idadi ya watumishi 2,957 wanohitajika ili kutekeleze majukumu ya Halmashauri hivyo kuna ipungufu wa watumishi 342 sawa upungufu wa asilimia 13.

2.2 Upungufu wa watumishi katika Halmashauri hii unachangiwa na sababu zifuatazo:-

- Hali ya usalama katika Wilaya hii kama ilivyokuwa inatangazwa na kuandikwa katika vyombo vya habari ilisababisha wataalam walioko sehemu mbalimbali nchini kuacha kuomba nafasi za kazi zinazotangazwa wilayani hapa.
- Kutokana na umbali wa wilaya hii kutoka sehemu mbalimbali bidhaa na huduma muhimu za viwandani kama vile vinywaji, vifaa vya ujenzi, mavazi, mafuta na vipuri na huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii zinafanya bidhaa hizo kuwa ghali kulinganisha na maeneo mengine nchini. Hivyo

watumishi wengi hasa wanaopata ajira kwa mara ya kwanza kutopendelea kuishi wilaya jirani ya Rorya.
- Ukosefu wa nyumba za makazi kwa watumishi na huduma nyingine muhimu za kijamii na kiuchumi ukilinganisha na Halmashauri nyingine,

2.3 Mkakakati.

Katika kupunguza tatizo la watumishi Halmashauri ina mikakati ifuatayo:
1. Kuendelea kuomba vibali vya ajira za watumishi wapya toka Wizarani.
2. Kuimarisha ulinzi na usalama na kuwaeleza watu kuwa hali ya ulinzi na usalama imeboreka ili kundoa hofu miongoni mwa watu kuwa Rorya ni sehemu isiyo salama.
3. Kuendelea kuwasiliana na serikali juu ya tatizo la upungufu wa watumishi na kuandaa mfumo wa motisha kwa watumishi wapya na waliopo.

3. HUDUMA ZA JAMII

3.1 Elimu

3.1.1 Idara ya Elimu ya Msingi

Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ina jumla ya shule za Awali 126 ikiwa shule 6 zinamilikiwa na taasisi binafsi na shule 120 ni za serikali. Aidha idadi ya wanafunzi wa awali ni 14,002 ikiwa wavulana ni 37,187 na wasichana ni 36,732 na Shule za binafsi zina idadi ya wanafunzi 808 ikiwa wavulana ni 426 na wasichana 382 na idadi ya wafunzi kwa ujumla 74,727 ikiwa 37,613 ni wavulana na 37,114 ni wasichana.

3.1.1.1 Ikama katika idara ya elimu msingi

Wilaya ina jumla ya walimu 1,414 miongoni mwao wanawake ni 858 na wanaume ni 556 na ina upungufu wa walimu 522 sawa na asilimia 27 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya walimu 1,936. Aidha, idadi hii ya walimu inajumuisha pia walimu wapya 302 walioripoti kwa mwaka 2015 kati ya walimu 320 waliokuwa wamepangwa kuripoti Wilaya ya Rorya na 18 hawakuripoti. Idadi hii ya walimu inajumuisha walimu wenye taaluma mbalimbali, ikiwa walimu wa III B/C 17, Walimu wa IIIA 1,354, Stashahada 40, Shahada 17 na Shahada ya uzamili 1. Kwa idadi hii ya walimu inafanya uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi kuwa 1:53

Zingatia Jedwali Na. 3a .

AINA YA WATUMISHI	MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU	% PUNGUFU
Watu ofisi ya afisa elimu msingi	12	7	5	42
Waratibu elimu Kata	26	26	26	-
Walimu	1,936	1,414	522	27
Wahasibu	120	-	-	-

AINA YA WATUMISHI	MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU	% PUNGUFU
Watunza stoo	120	-	-	-
Wapishi	120	-	-	-
Walinzi	120	-	-	-
Jumla	**2,172**	**1,451**	**553**	**69**

Samani za Shule za Msingi baada ya Kabla ya kutekeleza agizo la madawati Na. 3b

AINA YA SAMANI	MAHITAJI	ZILIZOPO	UPUNGUFU
Meza	3,120	1,809	1,311
Viti	3,120	1,350	1,770
Kabati	2,250	340	1,910
Shubaka	1,624	281	1,343
Madawati	24,690	18,542	6,148

Samani za Shule za Msingi baada ya kutekeleza agizo la madawati Na. 3c

AINA YA SAMANI	MAHITAJI	ZILIZOPO	UPUNGUFU
Meza	3,120	1,809	1,311
Viti	3,120	1,350	1,770
Kabati	2,250	340	1,910
Shubaka	1,624	281	1,343
Madawati	24,690	25,162	-

Majengo ya Shule za Msingi Na. 3d

AINA YA JENGO	MAHITAJI	YALIYOPO	UPUNGUFU
Madarasa	1,957	954	612
Nyumba za walimu	1,957	512	1,445
Matundu ya vyoo	2,937	1,059	1,915
Ofisi za walimu wakuu	236	202	34
Stoo	126	30	90
Vitabu vya kiada	596,874	286,415	310,459
Jumla	**5,906**	**288,967**	**314,285**

3.1.1.2 Changamoto

- Ucheleweshwaji wa mapokezi ya fedha za matumnizi mengineyo kutoka hazina, hivyo utekelezaji wa shughuli kuchelewa kuanza.
- Ufinyu wa bajeti
- Miundo mbinu ya shule mibovu

- upungufu wa samani.
- Upungufu wa walimu 343.

3.1.1.3 Utatuzi wa Changamoto

- Halmashauri kuendelea kuipa sekta ya Elimu kipaumbele katika bajeti zake,
- Kuendelea kuwasiliana na ngazi husika ili rasilimali zilizopangwa katika bajeti zipatikane kwa wakati

3.1.2 Elimu ya Sekondari

Wilaya ya Rorya ina jumla ya shule za sekondari 32 kati ya hizo shule za serikali ni 28 na binafsi ni 4 na Shule ya sekondari ya Nyanduga ni Shule ya pekee yenye kidato cha tano kwa Tahasusi za HKL, HGL ina wafunzi 52 ikiwa HKL 22 na HGL 30. Aidha idadi ya Wanafunzi katika shule za Serikali na Binafsi ni 10,808 kati ya hao Wavulana ni 6,212 na Wasichana ni 4,596 na idadi ya Wanafunzi katika shule za serikali ni 9,479 ambapo Wavulana ni 5,629 na Wasichana ni 3,850. Shule zisizokuwa za serikali zina jumla ya wanafunzi 1,329 ambapo Wavulana ni 583 na Wasichana ni 746.

3.1.2.1 Ikama ya watumishi Idara ya Sekondari

Wilaya ina jumla ya walimu 516 wakati upungufu ni walimu 138 hususan wa sayansi sawa na asilimia 21%. Idadi hii ya walimu inafanya uwiano wa walimu kwa wanafunzi kuwa 1:15.

Zingatia Jedwali hapa chini. Na. 4

AINA YA WATUMISHI	MAHITAJI	WALIOPO	PUNGUFU	% PUNGUFU
Watu ofisi ya afisa elimu Sekondari	7	4	3	42.9
Walimu	654	516	138	21
Wahasibu	28	-	-	100
Watunza store keeper	28	-	-	100
Wapishi	28	1	27	96.4
Walinzi	56	-	-	100
Jumla	**801**	**521**	**168**	**32.2**

Samani za Shule za Sekondari.

AINA YA SAMANI	MAHITAJI	ZILIZOPO	PUNGUFU/ZIADA
Dawati za wanafunzi	9479	9212	267
Viti vya wanafunzi	9479	9212	267
Meza za walimu	516	261	255
Viti vya walimu	516	337	179
Kabati	135	76	59

AINA YA SAMANI	MAHITAJI	ZILIZOPO	PUNGUFU/ZIADA
Shubaka	135	23	112

Majengo ya Shule za Sekondari.

AINA YA JENGO	MAHITAJI	YALIOPO	PUNGUFU
Madarasa	239	239	2
Nyumba za walimu	516	96	420
Jengo la Utawala	28	18	10
Matundu ya vyoo (wav)	225	139	86
Matundu ya vyoo (was)	193	116	77
Maabara	84	3	81
Mabweni	60	09	51
Bwalo	28	01	26
Kumbi za mikutano	28	01	26
Kasiki	28	27	1
Jiko	28	05	22

3.1.2.2 Ujenzi wa Maabara

Usimamizi, ukaguzi na ufuatiliaji wa ujenzi wa Maabara umeendelea kufanyika katika Shule za Sekondari. Hadi mwezi Octoba, 2016 ujenzi uko katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo; Maabara ambazo ujenzi uko hatua ya msingi ni 3, lenta 2, maboma 19, zilizoezekwa 40, kukamilika bila vifaa 17 na zilizokamilika kabisa ni 3.

3.1.2.3 Mikakati ya Ukamilishaji wa Maabara

- Kuendelea kusimamia na kuhamasisha jamii kuchangia nguvu kazi na fedha katika kukamilisha ujenzi wa maabara.

- Kuendelea kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo na sekta binafsi kuchangia ujenzi wa maabara.

3.1.2.4 Changamoto

- Upungufu wa Walimu 138 hususani walimu wa masomo ya Sayansi
- Upungufu wa Miundo mbinu na samani
- Ufinyu wa bajeti na fedha kutotolewa kwa wakati

3.1.2.5 Utatuzi wa Changamoto

- Kuazima walimu toka shule jirani na ni pamoja na kuajili walimu wa muda
- Halmashauri kuendelea kuipa kipaumbele sekta ya Elimu katika bajeti zake
- Kuendelea kuwasiliana na ngazi husika ili fedha tengwa zipatikane kwa wakati

3.2 Sekta ya Afya

Wilaya ya Rorya ina jumla ya vituo 41 vya kutolea huduma za Afya.
Vituo vimegawanyika Kama ifuatavyo:-

- Hospitali 3, Mashirika ya dini 2 ya Shirati (KMT) na Kowak (RC) na 1 katika taasisi binafsi.
- Vituo vya Afya 6
  - ❖ Vituo vya Serikali 3
  - ❖ Vituo vya Mashirika ya dini 3
- Zahanati 32 (serikali 24, Mashirika ya dini 3, binafsi 5)
- Vituo vya kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari 12. Aidha Halmashauri ya Wilaya inatengemea kufungua zahanati 7 na zahanati 3 ziko katika hatua ya ukamilishaji.
- Vituo vya kutolea dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (CTC) 6, katika vituo vya Shirati, Kowak, Changuge, Kinesi, Baraki Sisters na kituo cha afya RAO. Aidha katika mkakati wa ujenzi wa zahanati, Halmashauri ya Wilaya Rorya inajenga zahanati 5 zinazotegemewa kufunguliwa ifikapo juni 2015.

3.2.1 Changamoto

- Upungufu wa watumishi 51 hasa kwenye kada za Madaktari, Matabibu, Wateknoolojia wasaidizi maabara na Wauguzi
- Upungufu wa vituo vya kutolea huduma (Vituo vya Afya 20 na Zahanati 48)
- Upungufu wa dawa na vifaa tiba
- Upungufu wa nyumba za watumishi
- Upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Idara kwa mfano malipo ya stahiki za watumishi.

3.2.2 Utatuzi wa Changamoto

- Idara imekuwa ikishawishi wanachuo mfano Chuo cha Uuguzi Shirati kuja kuomba kazi na kuajiriwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya
- Idara imekuwa ikiweka kwenye mipango yake ujenzi wa zahanati na nyumba za watumishi na kuhamasisha jamii kuchangia katika miradi ya maendeleo.
- Uhamasishaji wa jamii katika kuchangia huduma za Afya katika mfuko wa
- Afya ya jamii ili kupata fedha kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

3.3 Sekta ya Maji

- ➢ Wilaya ya Rorya inatoa huduma ya maji safi na salama kupitia miradi ya visima, mabwawa, Malambo madogo, Miradi ya bomba na matanki ya uvunaji maji ya Mvua ampapo kuna miradi kumi na minne (14) inayoendeshwa kwa pampu na yenye mtandao wa mabomba (pumping & piped schemes) kati ya miradi hiyo, miradi minane (8) inafanya kazi. Wilaya ina visima 119. Kati ya hivyo visima 95 vinafanyakazi. Aidha Wilaya ina malambo 42 na mabwawa 6. Kiwango cha upatikanaji huduma ya maji Kwa sasa ni 45.03% ambapo watu wapatao 129,754 ndio wanaopata maji safi ya kunywa. Kiwango hiki ni chini ya lengo la kitaifa wa upatikanaji wa huduma ya maji vijiji ambalo ni asilimia

85 kwa maeneo ya vijijini na 95 kwa wakazi wa mijini. Aidha, kiwango cha upatikanaji kinatarajia kuongezeka baada ya kukamilika miradi inayoendela na ujenzi ya vijiji vya Kinesi, Randa, Utegi, Nyihara, Kisumwa, Mika na Nyamkonge, ukarabati wa miradi ya Marasibora, Komuge, Shirati na Ingrijuu na Kuendelea na ujenzi wa Miradi maalumu miwili ya Gabimori na Nyambori. Wilaya kwa asilimia 85 inategemea zaidi na vyanzo vya maji vya asili vifuatavyo:-

- Ziwa Victoria kwa wakazi wanaoishi kando ya ziwa
- Mito kama Mori na Mara kwa wakazi waishio kandokando ya mito
- Visima vifupi na virefu. Vyanzo hivi mbalimbali vilivyoendelezwa ni kama orodha inavyoonesha chini: -

Vyanzo vya maji Jedwali Na. 5

No	Aina ya chanzo	Idadi	Vinavyofanya Kazi	Visivyofanya kazi
1	Visima	119	95	
3	Mabwawa	5	5	-
4	Malambo madogo	42	42	-
5	Matanki ya uvunaji maji ya Mvua	8	8	-

3.3.1 Kamati na akaunti za maji vijijini zilizopo.

Kati ya vijiji **87** ni vijiji 31 tu ambavyo vina kamati na mifuko ya maji yenye thamani ya **Tsh.28,645,000**

3.3.2 Changamoto

- Mwitikio duni wa uchangiaji wa huduma ya maji kwa watumia maji, hivyo kuathiri uendelevu wa miradi ya maji (project sustainability)
- Mtiririko mdogo/ucheleweshwaji wa fedha katika kutekeleza miradi.
- Uhaba wa Rasimali watu (idara ina watumishi 3 ukilinganisha na mahitaji ya watumishi 27 kati ya watumishi waliopo 2 wanastaafu katika mwaka 2016/17.
- Uchakavu mkubwa wa miundo mbinu ya miradi ya maji iliyojengwa tangu mwaka 1972.

3.3.3 Utatuzi wa Changamoto

- Uundaji wa vyombo huru vya watumia maji ili kufanya miradi ya maji kuwa endelevu
- Kuendelea kuwasiliana na wazara ya maji juu ya utoaji wa fedha za wakandarasi wanaoendelea na ujenzi wa miradi
- Halmasahuri ina mpango wa kufunga power factor Correction device ili kupunguza matumizi makubwa umeme hususani kwa mradi wa maji Shirati.

4. SEKTA YA UZALISHAJI MALI

4.1 Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji

Kilimo kina nafasi kubwa katika kuinua uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Rorya. Eneo linalofaa kwa shughuli za kilimo na mifugo ni hekta 102,199. Eneo linalolimwa ni hekta 61,326 sawa na asilimia 60 ya eneo linalofaa. Eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 8,717. Eneo linalomwagiliwa kwa sasa ni hekta 1,039 sawa na asilimia 11.92 ya eneo linalofaa. Mazao ya chakula yanayolimwa ni mihogo mtama mahindi viazi vitamu maharage mpunga na ulezi. Mazao ya biashara ni tumbaku, Kahawa na mbaazi zimeanzishwa kama zao la biashara.

Wastani wa Uzalishaji wa Mazao mbalimbali. Na 6

NA	ZAO	LENGO (HA)	MAVUNO KISIWA (TANI)	WASTANI TANI/HA
1	Mahindi	11,332	31,720	2.8
2	Mtama	12,663	34,190	2.7
3	Mihogo	22,700	68,100	3.0
4	Viazi vitamu	11,332	33,996	3.0
5	Maharagwe	11,332	11,332	1.0
6	Ulezi	5,666	8,499	1.5
7	Karanga	4,533	4,533	1.0
8	Migomba	100	1,300	13.0
9	Mpunga	482	1,205	2.5
10	Kahawa	0	0	0.8
11	Pamba	0	0	0.7
12	Alizeti	28	45	1.6
13	Ufuta	13	21	1.6
14	Tumbaku	469	328	0.7

Chanzo: Idara ya Kilimo

4.1.1 Idadi ya zana za kilimo:

- Matrekta 50
- Plau za ng'ombe 45,622
- Majembe ya mkono 145,021
- Mikokoteni ya ng'ombe 35
- Matoroli 450
- Power tillers 23

4.1.2 Changamoto na Utatuzi Wake.

Pamoja na shughuli za kila siku za kiutendaji, kilimo kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

- Mwitikio mdogo na utayari wa wakulima kujishughulisha na kilimo hata kama huduma za ugani zinawafikia.
- Uhaba wa fedha za ujenzi na ukamilishaji wa miundo mbinu ya kilimo cha umwagiliaji
- Mitaji midogo ya wakulima kwa ajili ya kununua pembejeo na kuandaa mashamba
- Kutokuwepo kwa soko la ushindani kwa mazao ya biashara hasa tumbaku na mpunga
- Uwepo wa magonjwa ya mazao kama vile :
  - Mahindi (Maize Leathal Necrotic Disease –MLND) (.Elimu ya kupambana na ugonjwa huu inaendelea kutolewa.)
  - Mihogo (Batobato kali na michirizi kahawia).(Wilaya imeanza kuzalisha mbegu ya mihogo kinzani kwa kushirikiana na watafiti wa mihogo-Mikocheni.)
- Magugu hatari ya mazao kama vile Kiduha (Striga) kwa mazao ya mahindi na mtama (Elimu kinzani inaendelea kutolewa)
- Uhaba wa fedha za uendeshaji na usimamizi
- Uhaba wa vitendea kazi kwa maafisa na maafisa ugani.
- Mitaji midogo kwa vyama vya ushirika vya Akiba na Mikopo

4.2 Mifugo na Uvuvi:

Halmashauri inazo kaya 38,846 za wakulima na wafugaji kati ya hizo, kaya 27,718 zinajihusisha na ufugaji na zinakadiliwa kuwa na wastani wa ng'ombe 5 kwa kila kaya.Hata hivyo, Ufugaji ni shughuli muhimu inayoingizia wakazi pato katika Halmashauri. Aidha idadi ya mifugo imekuwa ikiongezeka kila mwaka, hadi kufikia 2013/2014 Halmashauri iliuwa na jumla ya mifugo 501,047 ukilinganisha na ile ya mwaka 2012/2013 ambayo ilikuwa na jumla ya mifugo 362,982 sawa na ongezeko la asilimia 28. Aidha mazao ya mifugo huchangia kipato cha familia na serikali kwa kuuza ngozi, maziwa na wanyama, kwa mwaka 2014 wastani wa mazao yatokanayo na mifugo yaliyouzwa ni kama ifuatavyo:-

- Ngozi za ng'ombe 2,612,
- Mbuzi1,788,
- Ngozi za kondoo 1,768
- Maziwa lita 68,761,440 zenye thamani ya Tsh 2,613,540,000/= zimezalishwa na kuuzwa.

Jedwali Na 7a. Linaonyesha ongezeko la mifugo.

Aina ya Mifugo	**2012/2013**	**2013/2014**
Ng'ombe	127,197	163,580
Mbuzi	74,513	97,577
Kondoo	34,329	41,483
Punda	813	1,657
Kuku	126,130	196,750
Jumla	**362,982**	**501,047**

Chanzo: - Idara ya mifugo

Jedwali Na. 7b Miundo Mbinu ya Mifugo

Aina	**Mahitaji**	**Iliyopo**		**Pungufu**
		Mizima	**Mibovu**	
Malambo	40	27	6	13
Majosho	40	20	11	8
Vituo vya afya ya mifugo/Uhamilishaji	6	2	2	2
Vichinjio	40	10	0	30
Maduka ya pembejeo	10	1	0	9
Vituo vya ukaguzi wa mifugo	4	1	0	3
Minada	3	3	0	0
Vibanio	40	3	0	37
Vituo vya kukusanya Maziwa	21	5	0	16
Jumla	**204**	**72**	**19**	**118**

Idara ya Mifugo – Rorya

4.2.1 Masoko ya mifugo

Halmashauri ina minada mitatu ambayo hutumika katika biashara ya mifugo:- Obwere, Randa na Nyamaguku.

4.2.2 Mafanikio ya Sekta

4.3 Uvuvi

Halmashauri ya Wilaya iko katika mwambao wa Ziwa Victoria, Uvuvi ni mojawapo ya shughuli muhimu ya kiuchumi huchangia 35% ya pato la Wilaya. Aidha Wakazi katika vijiji 23 na visiwa 3 walioko katika mwambao wa ziwa wanategemea uvuvi kama shughuli kuu katika maisha yao ya kila siku. Wakazi wanaojishughulisha na kazi ya uvuvi kila siku wanakadiriwa kuwa 6,817 wakiwa na mitumbwi ipatayo 2,105 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Hata hivyo, wapo wavuvi wanaotumia ndoano wanaokadiriwa kuwa 150 na hivyo kufanya jumla ya wavuvi wote kuwa 6,817. Wastani wa uzalishaji wa samaki ni tani 9,471 za Sangara zenye thamani ya shillingi 44,987,250/= kwa mwaka, Dagaa ni kilo 798,781 zenye thamani ya Tshs. 1,717,379,150 kwa mwaka na Sato tani 15.078 zenye thamani ya Tsh 67,851,000/= kwa mwaka.

4.3.1 Vikundi vya ulinzi wa rasilimali ya uvuvi na mazingira

Vikundi hivi maarufu kama “Beach Management Unit (BMU)” viko 32 kwa na vikundi hivi vinapatikana katika vijiji vyote 23 vilivyoko katika mwambao wa Ziwa Victoria kwa upande wa wilaya ya Rorya.

4.3.2 Idadi ya Mialo iliyoboreshwa

Mialo iliyoboreshwa kwa ajili ya kuuza samaki viwandani ni mitatu Nyang’ombe, Sota na Kibuyi.

4.3.3 Changamoto

- Ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa ajili ya ufuatiliaji.
- Uvuvi haramu wa kutumia zana haramu na sumu
- Kupungugua kwa usalama katika shughuli za uvuvi kunakotoka na na uvamizi wa maramia mara kwa mara ziwani.
- Upungufu wa boti kwa ajili ya doria na kukusanyia mapato.
- Kutopata fedha za kutosha kwa ajili shughuli za idara na za miradi ya maendeleo.
- Wafugaji kutokuwa tayari kuchangia gharama za utekelezaji wa miradi na hawawajibiki ipasavyo katika utunzaji wa miundombinu kama vituo vya kukusanyia maziwa na majosho.
- Mwitikio mdogo wa wafugaji kugharamia chanjo na matibabu ya mifugo yao.
- Watumishi kutolipwa stahili zao kama vile, uhamisho, likizo, kujikimu kwa ajira mpya.

4.3.4 Utatuzi wa Changamoto

- Kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya teknolojia mpya kwa wafugaji na wavuvi ikiwemo matumizi ya majosho na miundombinu mingine.
- Kuwaelimisha wafugaji kuwa sasa hivi gharama za chanjo na matibabu ni za wafugaji wenyewe na si za serikali tena kama ilivyokuwa zamani.
- Serikali kuleta fedha za ruzuku na za miradi ya maendeleo kama zinavyopangwa kwenye bajeti

4.4 Sekta ya Misitu

Halmashauri ya Wilaya ina upungufu mkubwa wa misitu kutokana uharibifu mkubwa wa mistu ya asili kutokana mahitaji ya miti kwa ajili ya mkaa, kuni na ujenzi. Pia ufyekaji wa misitu kwa ajili ya kilimo unafanyika kwa kiasi kikubwa. Mkakati ni kuhamasisha kila kijiji kuwa na bustani ya miche ya miti na kila kaya kupanda miti kuzunguka kaya na shamba la miti (woodlot) kwa matumizi ya nyumbani. Aidha katika kipindi cha mwaka 2014/2015 Halmashauri katika bajeti yake ilitegemea kupanda miti 1,500,000 hadi kufikia juni 2015 ilifanikiwa kupanda miti 996,467 sawa na asilimia 53 ya lengo. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 idadi ya miti iliyopandwa ni 1,020,889 ambayo ni sawa na 73% kati ya miti 1,500,000 iliyotakiwa kupandwa kwa mwaka.

4.5 Sekta ya Madini

Uchimbaji madini hufanyika kwa kiasi kidogo. Mchanga wenye aina ya madini yanayochimbwa ni dhahabu. Inatarajiwa kuwepo na uchimbaji wa madini katika Vijiji vya Chereche, Ochuna na Dett utakaoendeshwa na African Barick Gold Mine (Mwekezaji) baada ya utafiti kukamilika.

4.6 Ardhi, Maliasili na Mazingira

Wilaya ya Rorya ina miji midogo ya kibiashara ya Kinesi, Utegi na Shirati

Kituo cha na Mamlaka ya Mji mdogo Shirati. Miji hii ina jumla ya viwanja 2,348 vilivyopimwa kama ifuatavyo;

- Kituo cha biashara cha utegi Viwanja 162
- Kituo cha biashara Kinesi viwanja 124
- Kituo cha biashara Shirati viwanja 617
- Makao Makuu Ingri juu 1423
- Viwanja vinavyomilikiwa na tasisi za kidini vijijini 12
- Viwanja vinavyomilikiwa na taasisi za serikali vijijini 10

- Mashamba yaliyopimwa ni 14 yenye jumla ya hekta 4978.42 na mashamba 09 yamemilikishwa
- Vijiji vyote 80 vimepimwa mipaka
- Vijiji 62 tayari vimeandaliwa vyeti vya ardhi ya vijiji
- Vijiji vine (4) vya Nyambogo, Kitembe, Sudi na Sakawa vimeandaliwa mpango wa matumizi bora ya ardhi

4.6.1 Uundwaji wa Mabaraza ya Ardhi

Wilaya inayo Mabaraza ya Ardhi katika vijiji 87 na mabaraza ya Kata 26, mabaraza yanafanya kazi ya usuluhushaji wa migogoro ya ardhi. Aidha Wilaya ya Rorya haijaanzisha baraza la ardhi na nyumba la Wilaya, hivyo bado huduma zinaendelea kutolewa katika baraza la Ardhi na nyumba la wilaya ya Tarime.

4.6.2 Changamoto

- Upungufu wa watumishi 7 (wapima 3, watathimini 2, wachoraji ramani 2)
- Ukosefu wa vitendea kazi pamoja na rasilimali fedha
- Uelewa mdogo wa jamii katika masuala ya ardhi kunakopelekea kuwepo migogoro mingi ya ardhi
- Miundombinu isiyorafiki katika utekelezaji shughuli za kiidara.

4.6.3 Utatuzi wa Changamoto

- Kutoa elimu juu ya sheria ya ardhi No.4 na No.5 ya 1999 katika umilikishaji na uendelezaji ardhi za mjini na vijijini.
- Kuomba mamlaka ya serikali (Wizara ya Ardhi) kwa ajili ya uwezesho wa vifaa na vitendea katika idara.
- Kuendelea kuomba ajira za watumishi wapya kutoka menejimenti ya utumishi wa umma.

5. SEKTA YA HUDUMA ZA UCHUMI

5.1. Sekta ya Barabara

Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ina mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 699.5, kati ya hizo kilomita 161 zinahudumiwa na TANROADS Mkoa na kilomita 538.5 zinahudumiwa na Halmashauri. Aidha barabara hizo zimegawanyika katika makundi matatu:- Barabara za wilaya, Barabara za Mjini na Barabara za Vijijini. Km

498.4 ya barabara zinazohudumiwa na Wilaya ni za udongo na Km 130 ni za changarawe.

5.1.1. Changamoto

- Ucheleweshaji wa fedha /wakati mwingine kutopatikana kabisa katika utekelezaji wa shughuli za idara .
- Uhaba wa rasilimali 5 (Injinia 1, Mkadiriaji majengo1 na Mafundi Sanifu 3)
- Ukosefu wa vitendea kazi

5.1.2. Utatuzi wa Changamoto

- Kuendelea kuwasiliana na wizara kukumbushia kutolewa kwa fedha ili kutekeleza shughuli za idara
- Kuendelea kuwasiliana na TAMISEM ili kuajili watumishi wanaohitajika ili kutekeleza majukumu ya idara kwa ufanisi

5.2. Huduma za ndege

Wilaya ina kiwanja kidogo cha ndege (Air Strip) katika mji mdogo wa Shirati

5.3. Huduma za Mawasiliano

- Kuna Kituo kimoja cha Shirika la Simu Tanzania (TTCL) katika mji mdogo wa Shirati. Huduma za simu za mkononi zinatolewa na makampuni ya VODA, TTCL, Airtel, TIGO na Halotel katika katika maeneo yote ya Wilaya.

5.4. Huduma za umeme.

Inapatikana katika njia za Utegi – Shirati, Kinesi – Kibuyi, Kuruya – Kinesi, Tarime Kirumi na Kinesi – Utegi.

5.5. Huduma za Bandari

- Bandari ya Kinesi na
- Bandari ya Ruali

5.6. Taasisi za Fedha

Wilaya ya Rorya wakazi wake hupata huduma za fedha kutoka Makao Makuu, Shirati na Tarime kupitia taasisi za fedha zifuatazo: NMB tawi la Shirati na Rorya , Benki ya CRDB tawi la Tarime na Rorya vilevile benki za NBC, POSTA zenye matawi yake Tarime na mashirika ya kifedha ya Bay port, FINCA NA PRIDE yenye makao yake Tarime na SACCOS 7

6. Idara ya fedha na Biashara

Idara ina jumla ya watumishi 12, ikiwa wahasibu 8 wasibu wasidizi 2 na Mkuu wa idara/mtunza hazina 1 walioko katika Makao Makuu ya Walaya na mhasibu1katika Mamlaka ya mji mdogo Shirati, hata hivyo katika kukamilisha ikama ya idara bado ina upungufu wa mtumishi 14 ili kuwa na watumishi 26.

6.1. Changamoto

- Upungufu wa vitendea kazi
- Chumba mdhubuti cha kutunzia nyaraka za fedha
- Ukosefu wa umeme wa uhakika
- Upungufu kwenye mfumo wa malipo (mitandao hafifu ya mawasiliano)
- Ukosefu wa usafiri wa uhakika kwenye ukusanyaji wa mapato

6.2. Utatuzi wa Changamoto

- Halmashauri inatafuta usafiri wa uhakika kuwezesha ufanisi kwenye mapato, kuongeza vitendea kazi vya idara kama viti, meza kupatikana kwa genereta na chumba maalum kwa ajili ya kutunzia nyaraka za fedha.

7. Kitengo cha ukaguzi wa ndani wa hesabu.

Kitengo cha ukaguzi wa ndani nimiongoni mwa vitengo 6 vya Halmasahuri ya Wilaya ya Rorya kilicho pewa Mamlaka ya kukagua na kuandaa taarifa za ukaguzi kwa kila robo mwaka na mwaka kwa ujumla wake na kuwasilisha katika mamlaka husika.Kitengo hiki kina jumla ya watumishi 2 kati ya watumishi 3 wanaohitaka.

-

7.1. Changamoto

- Upungufu Rasilimali watu katika kitengo, hivyo kupunguza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kitengo
- Ukosefu wa rasilimali fedha hata wakati mwingine kutopokelewa kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

7.2. Utatuzi wa Changamoto

- Kuendea kuwasiliana na Wizara ya Ofisi ya Rais utumishi wa umma kuongeza watumishi katika kitengo.
- Kuendelea kuwasiliana na serikali kutoa ruzuku ya matumizi mengineyo OC ili kitengo kiweze kupanua wingo wa ukaguzi na usimamizi wa matumizi bora ya fedha na utwala bora.

8. Kitengo cha Manunuzi

Kitengo cha manunuzi ni miongoni mwa vitengo vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kwa madhumini ya kusimamia utekelezaji wa manunuzi ya Serikali kwa kufuta Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2011. Aidha kitengo kina jumla ya watumishi 6, hivyo kuwa na upungufu wa mtumishi 1 ili kukamilisha idadi ya watumishi 7 wanaohitajika.

8.1. Changamoto

- Ukosefu wa Ghara (store) kwa ajili ya kuhifadhi Mali za Serikali.
- Ukosefu wa Vitendea kazi, kam vile samaini za ofisi, kompyuta, Printa, Photokopi na mifumo ya kielectroniki.

- Ufinyu wa bajeti katika kitengo, hivyo kufanya kitengo kutotekeleza majukumu yake kwa ufanisi

8.2. Utatuzi wa Changamoto

- Halmashauri kuendelea kuweka kipaumbele katika mpango na bajeti za ujenzi wa ghala la kuhifadhia nyaraka za serikali.
- Halmashauri inaendelea kutafuta vyanzo vya fedha ili kununua vitendea kazi ni pamoja na kununua pikipiki ili kusaidia usambazaji wa Mikataba na ufuatiliaji wa nyaraka mbalimbali za serikali katika maeneo yake.

9. Kitengo cha Sheria

9.1. Kazi za idara/Majukumu

- Kutoa ushauri wa kisheria katika Wilaya
- Kuendesha kesi zenye utata au ubishini wa kisheria katika Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.
- Kuwakilisha wilaya katika mikutano mbalimbali yene mlengo wa kisheria.
- Kusimamia, kufuatilia na kutoa ushauri katika Mabaraza ya Kata

9.2. Changamoto

- Upungufu wa Mwanasheria1.
- Ufinyu wa bajeti katika kuendesha kitengo
- Wilaya kutokuwa na Mahakama ya Wilaya hivyo kulazimu kesi zote kuendeshwa nje ya wilaya.

9.3. Utatuzi wa Changamoto

- Kuendea kuwasiliana na Wizara ya Ofisi ya Rais utumishi wa umma kuongeza watumishi katika kitengo

10. Kitengo cha Mawasiliano/TEHAMA

Kitengo kilianzishwa rasmi katika halmashauri ya Rorya mwaka 2012. Kitengo kina watumishi 2 kati ya watumishi 6 wanahohitajika. Kina majukumu ya kusimamia miundombinu ya mawasiliano ndani ya halmashauri, kutoa ushauri mzuri kwa Mkugenzi Mtendaji (W) juu ya matumizi mema ya miundombinu ya mawasiliano, kusimamia shughuli ya kukusanya na kutunza habari na matukio ya halmashauri hasa ya vikao vya halmashauri.

10.1. Changamoto

- Ikama ya watumishi wa kitengo haijakamilika, hasa Afisa Habari,

- Ukosefu wa vitendea kazi kama kompyuta, printa, photocopy, kamela, simu, vifaa vya kuunganishia na kufungua mifumo yani fundi vifaa vyo kompyuta (Kiti ya vifaa vya TEHAMA).
- Bajeti finyu ya kuendeshea shughuli za kusimamia mifumo

10.2. Utatuzi wa Changamoto

- Kuweka katika bajeti maombi ya watumishi kwa menejimenti ya utumishi ya Umma.
- Maombi ya vitendea kazi kupitia bajeti Halmashauri na wadau.
- Kitengo kuongezewa bajeti na kuletwa kwa wakati.

11. Idara ya Mazingira

Idara ina jumla ya watumishi 12 ikiwa na maafisa afya 7, wasaidizi wa afya 4 na Mkuu wa idara 1. Walioko Makao Makuu ya Walaya 4, ngazi ya tarafa 4, hivyo katika kukamilisha ikama ya idara bado ina upungufu wa mtumishi 31, ikiwa Maafisa Afya 8, Maafisa afya wasaidizi 22 na Afisa mazingira 1 ili kukamilisha jumla ya watumishi 43.

11.1. Changamoto

- Upungufu wa watumishi 31(Maafisa Afya 8, Maafisa afya wasaidizi 22 na Afisa mazingira1)
- Ukosefu wa vitendea kazi vya ukusanyaji wa taka ngumu na maji
- Uchafuzi wa mazingira hususan katika sehemu za umma.

11.2. Utatuzi wa Changamoto

- Kuweka mapungufu ya watumishi katika ikama wakati wa bajeti.
- Maombi ya vitendea kazi kupitia bajeti na wadau mbalimbali wa maendeleo
- Uhamasishaji jamii kutunza mazingira.

12. Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji

Hamashauri inayo Mipango ya Maendeleo ya Muda wa Kati na Muda Mrefu kama: Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano 2015-2020, Mpango Mkakati wa Halmashauri (SP) 2015-2020. Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/17 (MTEF). Aidha Halmashauri inakusanya, inachambua, inatunza, inasambaza Takwimu na taarifa za maendeleo kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya wilaya. Mifumo wezeshi katika kufanikisha azma hii ni pamoja na PLANREP, LGMD, TOMSHA, OPRAS, MTUHA. DROMAS na EPICOR.

Idara ina jumla ya watumishi 4 ikiwa na wachumi 3 naMtakwimu 1 ambao wamegawanyika katika viengo vya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji.

12.1. Kazi /Majukumu za idara

- Kufanya utafiti na kubainisha fursa za uwekezaji zilizopo katika Wilaya (Project Writt up)

- Kuchambua, kuandaa na kusimamia mpango na bajeti ya Wilaya (Budget and planning scruitinization and Preparation)
- Kuandaa na kuratibu mpango kazi wa Wilaya (Action plan)
- Kubuni na kuweka mikakati ya kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa wananchi.
- Kuchambua takwimu na taarifa mabalimbali za kiuchumi na kuandaa sera za kiuchumi kwa ujmla na mipango ya maendeleo ya .
- Kuandaa mifumo/Mitindo ya uchambuzi wa makisio na vigezo vya uchumi.
- Kufanya ufutiliaji na usimamizi na tathimini ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.
- Ukusanyaji, uratibu na uchambuzi na usambazaji wa takwimu za kijamii na kiuchumi.

12.2. Changamoto

- Uhaba wa rasilimali fedha katika kutekeleza majukumu ya msingi
- Upungufu wa vitendea kazi hivyo kuzoofisha ufanisi wa kazi.
- Miradi ya Maendeleo kutokamilika kwa wakati na viwango vinavyotakiwa.
- Ukosefu wa Huduma za inteneti za kuaminika katika Makao Makuu ya Wilaya.

12.3. Utatuzi wa Changamoto

- Kuimarisha uratibu katika utendaji kazi za halmashuri ili kuongeza ufanisi katika matumizi ya rasilimali chache zilizopo..

13. Sekta ya Maendeleo ya Jamii

Idara ina jumla ya watumishi 17 (Me 8 na Ke 9). Kati yao, watumishi saba wako Wilayani na watano wako ngazi ya Kata.

13.1. Vikundi vya Uzalishaji Mali.

Wilaya ina jumla ya vikundi 520 vinavyojishughulisha na uzalishaji mali katika nyanja za kilimo, ufugaji, biashara, ufinyanzi, ususi, ufumaji, usindikaji, utengenezaji batiki, utengenezaji sabuni, mafuta na uselemala. Aidha Vikundi hivi vinapata mikopo kutoka serikali kuu, Halmashauri na mashariki ya fedha kama vile mara women, Empowerment Assistance (MWEA) FINCA na PRIDE. Wananchi wapatao 10,400 wamejiunga katika vikundi vya kuweka na kukopa (VICOBA).

13.2. Watoto wanaoishi katika mazingira magumu (WWKMM), wazee na walemavu.

Wilaya ya Rorya ina jumla ya watoto 13,759 (ikiwa 7,983 me na 5,458 ke) wanaoishi katika mazingira magumu na jumla ya Wazee 31,759 (ikiwa 17,462 KE na 14,279) na walemavu 832 (ikiwa 503 me na 329ke). Aidha pamoja na misaada toka serikali kuu yapo mashirika yasiyo ya kiserikali yanayojihusisha na utoaji wa misaada kwa Watoto wanaoishi katika mazingira magumu (WWKMM), kama vile Mkomboe, Grobal

Resource Alliance (GRA), Teachers Good Will foundation, Compassion PACT - TANZANIA.

13.3. Hali ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI.

Kutokana na utafiti uliofanywa mwaka 2011/2012 na THMIS kiwango cha maambukizi ya VVU katika Wilaya ya Rorya kimeshuka kutoka 13.7% (RAS MARA THMIS 2008) kufikia 6.2% (Ras mara / this 2012)

Kiwango cha maambukizi kimepungua kutokana naj itihada mbalimbali zilizofanywa na wilaya kwa kushirikiana na wadau, hata hivyo bado kiwango hicho kiko juu ya kile cha kitaifa. Mikakati ya Wilaya ni kuendelea kutoa elimu ya kinga dhidi ya VVU na kupinga ukatiri wa kijinsia ambao pia umekuwa ni kichocheo kikubwa cha kueneza maambukizi ya virusi vya Ukimwi/Ukimwi kwa kushirikiana na Asasi za kirai kama vile KMT, CSSC, KKKT, BEIRA, MVIWANYA . Aidha wilaya itaendelea kutoa elimu ya kinga dhidi ya UKIMWI kwa njia ya mikutano, semina na makongamano, kutumia waelimishaji rika, Klabu za Ukimwi mashuleni, Vikundi vya wasanii, huduma za WAVIU, na usambazaji wa kondom katika maeneo hatarishi kama vile Mialo, Minada Maeneo ya miji midogo inayokua na masoko.

13.4. Changamoto

- Vitendo vya ukatili wa kijinsia vimeongezeka
- Uhaba wa rasilimali fedha kama mitaji kwa vikundi
- Vikundi kuwa tegemezi.
- Uhaba wa rasilimali watu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya idara.
- Mira na desturi potofu kwenye jamii husika.

13.5. Utatuzi wa Changamoto

- Elimu ya ukatili inaendelea kutolewa kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserekali
- Kuendelea kuhamasisha wanavikundi kujenga moyo wa kukuza mitaji yao.
- Kuendelea kutumia mfuko wa wanawake na vijana kuoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana na wanawake.

14. Mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF).

Wilaya Rorya ni miongoni mwa Wilaya zinazotekeleza Programu ya Mfuko wa maendeleo ya Jamii (TASAF). Hadi kufikia Juni 30, 2016 Programu hii imeweza kuhawilisha jumla Tsh1,555,112,000 kwenda kwenye kaya masikini 7,363. Fedha hizi zimetumika kwa Maandalizi ya watoto kwenda shule, kuanzisha biashara ndogo ndogo, watoto kwenda kliniki, kununua mbegu bora kwa ajili ya kilimo, kulipa ada ya kujiunga na mfuko wa bima ya Afya (CHF) na usimamizi, ufutiliaji na kuhawilisha fedha na ujazaji wa fomu za madai, mafunzo ya kujenga uelewa na kuwezesha jamii kubadili mtizamo juu ya matumizi sahihi ya fedha na kuwajengea uwezo wa kujitegemea pindi mradi ukifikia ukomo wake.

14.1. Changamoto

- Dhana ya kaya masikini haikufamika vema kwa wananchi wengi, hivyo hudhani masikini ni kundi la wazee, walemavu na wagonjwa
- Kutokuwepo kwa mabadiliko ya mfumo wa usajili wa wanafunzi wa darasa la 7 kwenda kidato cha kwanza.
- Malalamiko ya vijiji 35 na kaya 30 zinahitajika kuingizwa katika programu.

14.2. Utatuzi wa Changamoto.

- Elimu kutolewa kwa jamii kuhusu dhana ya kaya masikini ni zile kaya zisizo kuwa na uwezo wa kiuchumi ambazo zikiwezeshwa zitaweza kujikwamua kiuchumi.
- Marekebishi ya mfumo wa (PSSN) ili kuendena na mabadiliko ya wanafunzi wa darasa la 7 kwenda kidato cha kwanza.
- Kuendelea kuwasiliana mratibu wa program kitaifa kuingiza Vijiji 35 na kaya 30 katika mpango.

15. Uendelezaji wa Makao Makuu ya Wilaya

Hadi kufikia hivi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imepokea pesa za undelezaji wa makao zaidi bilioni 3 ambazo zilitumika katika ujenzi wa ofisi na nyumba 8 za watumishi na sasa Halmashauri inaendelea na ujenzi wa ukumbi wa mikutano na ujenzi umefikia hatua ya msingi. Bado jitihada zaidi zinahitajika katika ujenzi wa miundombinu muhimu inayohitajka ikihusisha; Hospitali, masoko, nyumba za watumishi 77, barabara za mitaa na mtandao wa maji.

16. HITIMISHO

16.1. Changamoto za maendeleo zinaoikabili wilaya

- Ufinyu wa bajeti na ucheleweshaji wa fedha toka hazina zilizoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza shughulu mbalimbali/majukumu.
- Uhaba wa rasilimali watu hivyo kufanya Halmashauri kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
- Mwitikio mdogo na kipato kidogo kwa wananchi hivyo kushindwa kuchangia Miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika ngazi za chini.
- Ukusanyaji mdogo wa mapato ya ndani.
- Uhalifu, ujambazi/wizi wa mali kama Mifugo na mali za wavuvi na uvuvi haramu unao fanywa na baadhi Raia wa Nchi jirani za Kenya na Uganda.
- Wzalishaji mdogo wa mazao ya chakula na biashara
- Kiwango kikubwa cha maambuki ya VVU
- Upungufu mkubwa wa watumishi hususan, katika sekta za maji, Afya, Elimu, Kilimo, Mifugo, Uvuvi na maliasili.

16.2. Katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wilaya inaendelea kufanya juhudi zifuatazo:-

- Kuhamasisha jamii ili kukusanya vifaa vya ujenzi hususan Matofari, mawe, mchanga na kokoto ili kuisijitokeze tatizo la upungufu wa vifaa vya ujenzi kukwamisha utekelezaji wa miradi pindi fedha zitakapokuwa zimetolewa.
- Kuhamasisha jamii kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo vijijini kwa kutumia watumishi wa ugani.
- Kuendelea kuomba vibali vya ajira za watumishi wapya toka Wizara ya Utumishi na kuendelea kuwasiliana na hazina kupitia ofisi ya TAMISEMI ili waweze kuzingatia mtiriko wa fedhakama ulivyo pangwa.
- Kujenga uzio katika minada ya mifugo kwa kuanza na midada ya Nyamuguku na Obwere ili kuepuka upotevu wa mapato.
- Kuhahikisha kuwa suala zima la ulinzi na usalama linasimamiwa na kuboresha ili kuweza kuweka mazingira bora ya uwekezaji.
- Kuhamasisha jamii ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara